

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
21 Juni 2008**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Markus Weise
Mussa Alex
Mussa Omari
Paulo Atibu Hatibu
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

Mradi wa usalama barabarani - Wamba Memorial Fund

Wakati wa wiki Markus na Juma walijaribu kwenda kwa shule za Kigamboni pamoja na HUWATA kama walivyopanga lakini jumanne HUWATA walikuwa na mkutano mwingine, jumatano hawakuwepo ofisini na ijumaa hawakuwepo ofisini. Jumamosi walimpa Juma orodha ya shule tano pamoja na kiasi cha wapanda baisikeli kwenye kila shule.

Elaine hajakuwa na nafasi kuanza kutafsiri manual.

Jumatatu Markus and Juma walimpa Bwana Wemba wa Chuo cha Usafirishaji nakala ya manual ili atoe maoni yake.

TANROADS na barabara mpya

Elaine aliandika barua kwa TANROADS kuomba taarifa ya njia za baisikeli zipo wapi sawa sawa kwenye barabara ya Sam Nujoma na barabara ya Kilwa, na Markus na Juma walileta barua ofisini kwa TANROADS ijumaa. Walipendelea tuongee na consultants na contractors.

Tuliongeana kwamba inaonekana tunaangaika tu kwa sababu zamani tuliambiwa na contractors na consultants kwamba bora tuwasiliane na TANROADS. Wanachama walitoa mawazo kwamba tupate msaada wa Diwani Lupilya na labda yeye atasikilizwa zaidi. Lakini shida ni kwamba yeye ni diwani wa Ilala na barabara zipo Kinondoni na Temeke. Tulikuwa na wazo kwamba yeye anaweza kutusaidia kuomba mkutano na meya wa jiji la Dar es Salaam.

Kodi

Elaine aliandika upya barua kwenda TRA kama tulivyokubaliana na Markus na Juma waliletea TRA jumanne na walifuatalia alhamisi.

Umoja wa Ulaya

Markus na Juma walifuatalia barua tuliyoandika kwa Umoja wa Ulaya mwezi wa kwanza mwaka huu, ambayo bado hatujapata jibu. Askari hawakuruhusu waingie jengo, na waliambiwa wa pige simu kupata appointment. Walipiga simu na waliambiwa na mtu anaitwa Anna atawapigia simu baadaye, lakini hakuwapigia. Walipiga simu tena na alisema kwamba kila mtu kwenye Umoja wa Ulaya yupo likizo. Waliacha nakala nyingine ya barua na askari.

Ofisi

Juma alipendelea tuandike barua kwa serekali ya mtaa ya Manzese kututambulisha, na kwa serekali ya mtaa ya Mabibo kueleza kwamba tunahama.

Mejah bado hajapaka rangi nembo yetu ofisini.

Mambo ya hela

Juma alipata Tsh 21,000 kama kodi ya guta kwa wiki tatu. Alitumia Tsh 2,000 kwa marker pens na Tsh 1,800 kwa vifaa vya ofisi. Sasa ana Tsh 63,700 ya hela ya UWABA.

Tumemwaga Markus

Hii ilikuwa mkutano wa mwisho wa Markus. Wanachama walimshukuru sana kwa ajili ya kazi ameyofanya, msaada ameutoa kufuatalia mradi wa Wamba pamoja na uboresho wa mazingira ya wapanda baisikeli Dar es Salaam, na mawazo ameyochangia. Wanachama waliandika barua za kushukuru awenazo kama kumbukumbu na tulipiga picha za pamoja.

Markus alitangaza kwamba anachangia hela ya Tsh 450,000 kwa UWABA na ameshaiweka kwenye akaunti ya benki ya UWABA. Inawezakutumkiwa kwa ajili ya fanacha kwa ofisi mpya, na kununua guta nyingine kuongeza mapato yetu. Wanachama walimshukuru sana ya mchango wake kubwa.